

Jinsi ubunifu wetu unavyobadilisha mandhari nchini Kenya na kwingineko

Mpira wa mbegu ni mbegu tu ndani ya mpira wa vumbi la mkaa uliochanganywa na nyenzo zenyenye virutubisho, ambazo hutawanywa shambani.

Upandaji wa moja kwa moja wa mbegu hupunguza mshtuko wa kupandikiza na husaidia miti michanga kupata mizizi yenyenye nguvu ambayo nayo huimarisha miti ardhini. Hata hivyo, matumizi ya mpira ya mbegu husaidia kulinda mbegu kwa njia ya asili isiyo na sumu. Mkaa hutumika kulinda mbegu hadi mvua inyeshe, ioshe mkaa na mbegu iwe wazi. Hii ni kupunguza ghamama za kupanda aina mbalimbali muhimu za mimea ya kiasili na kuzuia mbegu kuliwa na ndege, utitiri na kindi.

Matumizi ya mkaa

Vumbi la mkaa hutumika kutengeneza mpira ya mbegu ili kuzilinda dhidi ya ndege, utitiri na kindi. Pia ni bora kwa udongo.

Kwa kuwa miti hukatwa kutengeneza mkaa, matumizi ya vumbi la mkaa kutengeneza mpira ya mbegu husaidia kukamilisha mzunguko wa nishati ya mkaa.

Usambazaji wa mbegu

Aina za miti zinazochaguliwa kutengeneza mpira ya mbegu ni zile zinazotumiwa sana kutengeneza mkaa. Hizi ni pamoja na acacia tortillias, acacia syel, quesadilla, nylotica.

Mbegu hutawanywa mashambani kwa kutumia parachuti., helikopta, ngamia, watu n.k.

Changamoto za mbinu hii ni kwamba miti huchukua muda mrefu kukua.